

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA.

(SURA 287)

SHERIA NDOGO

(zimetungwa chini ya kifungu cha 153)

**SHERIA NDOGO ZA (KUZUIA UHARIBIFU WA BARABARA) ZA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA MWAKA 2017**

- | | | |
|----------------------------|---|--|
| Jina na tarehe ya kutumika | 1 | Sheria ndogo hizi zinaitwa sheria ndogo za (kuzuia uharibifu wa barabara) Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za mwaka 2017 na zitaanza kutumika mara zitakapotangazwa kwenye gazeti la Serikali. |
| Eneo la kutumika | 2 | Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. |
| Tafsiri | 3 | <p>Katika sheria hizi isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo;</p> <p>“Afisa mwidhiniwa” maana yake ni Mhandisi wa Ujenzi, Afisa ardhi, Mwanasheria au afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi.</p> <p>“Barabara za Halmashauri” ni barabara zilizotengenezwa na Halmashauri katika maeneo yake na kukabidhiwa kwa wanakijiji husika kwa ajili ya kuitumia na kuihifadhi ipasavyo.</p> <p>Barabara za Kijiji/ vijiji ni barabra iliyochimbwa/ iliyotengenezwa ndani ya kijiji au kuelekea kijiji jirani na wananchi nguvu kazi wa kijiji husika kwa manufaa ya kijiji.</p> <p>“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.</p> <p>“Mkurugenzi” maana yake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa au afisa yeyote anayekaimu nafasi hiyo kwa wakati huo.</p> |

Matumizi sahihi
ya barabara

- 4 Matumizi sahihi ya barabara ni pamoja na;
- (a) Mtembea kwa miguu au mwendesha gari, pikipiki, baiskeli kuhakikisha kuwa anapokuwa barabarani anafuata alama za barabarani ikiwani pamoja kupita upande anaopaswa kupita.
 - (b) Kutunza barabara kwa kuzuia kutupa takataka maeneo ya barabarani.
 - (c) Kuzuia mifugo kupita barabarani.
 - (d) Kuhakikisha kuwa magari hayapiti katika barabara za watembea kwa miguu.
 - (e) Kuzuia shughuli za kilimo katika eneo la hifadhi ya barabara,
 - (f) Gari lenye uzito wa tani kumi tu litakuwa na uwezo wa kupita katika barabara za Halmashuri.
 - (g) Kufyeka nyasi katika barabara pale inapohitajika kufanya hivyo,
 - (h) Kufukua mifereje kando ya barabara inapokuwa na mchanga,

Ukaguzi wa
barabra

5. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na jukumu la
- (a) kukagua uzito wa gari katika barabara;
 - (b) Mageti/ vizuizi vilivyowekwa barabarani na Halmashauri vitakuwa ni vituo vya kukagua uzito wa gari.

Ukubwa wa
barabara

- 6 Ukubwa wa eneo la Barabara katika Halmashauri utakuwa kama ifuatavyo;
- (a) Barabara zinazounganisha Wilaya na Mkoa zitakuwa na upana wa mita tano na nusu (5.5)
 - (b) Barabara zinazounganisha Vijiji, kata na wilaya ni mita tano na nusu (Feeder roads)
 - (c) Barabara za jumuiya zinazounganisha Mtaa na mtaa au kitongoji na kitongoji ni mita tano na nusu (5.5) (community roads)

Hifadhi ya
barabra

- 7 Upana wa barabara mbalimbali pamoja na hifadhi yake utakuwa kama ifuatavyo;
- (a) Barabara kuu za mkoa ni upana wa mita sitini (60) kutoka katikati ya barabara ni mita thelathini kwa kila upande.
 - (b) Barabara zinazounganisha Wilaya na mkoa ni upana wa mita arobaini (40), kutoka katikati ya barabara ni mita Ishirini kwa kila upande.
 - (c) Barabara zinazounganisha vijiji, Kata na Wilaya ni Upana wa mita thelathini (30), kutoka katika ya barabara ni mita Ishirini kwa kila upande.
 - (d) Barabara za jumuiya zinazounganisha mtaa na mtaa au kitongoji na kitongoji ni upana wa mita ishirini na tano (25) ,upana kutoka katikati ya barabara ni mita kumi na mbili nna nusu kwa kila upande.

- Usimamizi wa barabara 8 Afisa mwidhiniwa wa Wilaya na wa ngazi ya kata na kijiji atakuwa ndiye msimamizi mkuu wa matumizi sahihi ya barabara.
- Makosa 9 Mtu yeyote atakuwa amevunja sheria ndogo hizi endapo;
- (a) Atapitisha gari lenye uzito wa zaidi ya tani kumi katika barabara za Halmashauri.
 - (b) Atapitisha mifugo barabarani au kuchimba barabara.
 - (c) Atafanya shughuli mbalimbali katika eneo la hifadhi ya barabara kama vile kujenga, kulima, kukata miti, kufyatua tofari au shughuli yeyote ile.
 - (d) Atangushia miti kando ya barabara, kuweka magogo, kufyeka nyasi katika eneo la hifadhi ya barabara pale litakapokuwa na nyasi ndefu.
 - (e) Ataacha gari bovu barabarani.
 - (f) Atafanya kitu chochote tofauti na matumizi sahihi ya barabara.
- Adhabu 10 Mtu yeyote ambaye atakiuka au kwenda kinyume na sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungu shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi mia tatu elfu, au kifungu kisichopungua miazi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa umebandikwa katika sheria ndogo hizi
kufuatia mkutano wa baraza la madiwani uliofanyika
tarehe.....mwezi.....2011 mbele ya ;

.....
ROBERT MASUNYA
MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYAYA IRINGA.

.....
STEPHEN MHAPA
MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA.

NAKUBALI

.....
MHE. GEORGE B.SIMBACHAWENE (MB)
WAZIRI WA NCHI –OR-TAMISEMI

DODOMA,

TAREHE.....MWEZI.....2017.